

Pambazuko

Toleo Namba 058

Jumatatu Januari 22-28, 2024

**Iweje CCM
wajitwike mzigo
wa ubaya?... Uk.5**

**Dakika 28,
Tanesco yakata
umeme mara
81... Uk.8**

**Nani hasa
anapanga
kumuua
Kigwangalla?**



Habari kamili Uk.6

UGANDA

**Museveni
mwenyekiti
mpya
wa G77
Uk. 17**

KENYA

**Kenya
yasema
haina vita
na majirani
Uk. 16**

CONGO

**Walenzi UN
waanza
kuondoka
DR Congo
Uk. 10**

RWANDA

**Wakimbizi
Rwanda
marufuku
Uingereza
Uk. 19**

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

Tahariri

Nani hana usingizi akiwapigania Watanzania?

TUMEKUWA tukiambiwa kwamba Rais Samia Suluhu Hassan anakosa usingizi kwa kuwa anawaza na kuwazua afanye nini ili kupunguza madhila ya wananchi anaowaongoza – Watanzania.

Inawezekana kuna ukweli wa maneno hayo yanayotoka kwa wasaidizi wake, ingawa inaleta ukakasi kidogo kwa kuwa yanatolewa na wanasiasa wetu ambao tunawafahamu hulka na mienendo yao; kupenda kujipendekeza na mara nyingi kusema uongo.

Imani ya wengi ni kwamba kuna asilimia kadhaa ya ukweli kwenye maneno hayo kutokana na ukubwa na ugumu wa kazi ya kuongoza wananchi wengi masikini - idadi kubwa wakikosa kujua watakula nini kwa mlo unaofuata, baada ya kubahatisha mmoja kwa shida.

Pamoja na imani hiyo kwa Rais Samia, hatuna uhakika endapo kuna waziri hata mmoja, anayekosa lepe la usingizi kwa kuwahurumia Watanzania.

Mawaziri wengi tunawaona wakipuyanga tu na kujifanya wako “bize” kutumikia wananchi, lakini matokeo yake hatuyaoni.

Madhila mengi katika wizara yapo kwa kuwa mawaziri wengi hawawajibiki ipasavyo. Kwamba hawafanyi kazi zao kwa ufasaha, hawatumii muda na uwezo wao wa kufikiri kutatua kero lukuki za wananchi.

Hivi sasa maeneo mengi ya Tanzania tunashuhudia- baada ya miaka 60 ya uhuru, bado kuna shida kubwa ya maji, licha ya kuwa na vyanzo vingi vya kupatikana kwa maji, tena kwa gharama nafuu

zaidi.

Maeneo mengi ya vijijini yana hali mbaya zaidi kwa kukosa maji safi na salama, hivyo binadamu kulazimika kutumia maji yanayoogeshwa na ama kunyweshwa wanyama. Hii ni aibu kubwa.

Mbali na vijijini, maeneo mengi ya mijini na hata majiji, bado kuna shida kubwa ya maji. Wananchi wanalazimika kutumia fedha nyingi kununua maji kutoka kwa wafanyabiashara wanaouza maji bei aghali mno – kwa kuwa wanatambua hakuna mbadala wake.

Kwamba hata katika maeneo mengi, na hata mijini kwa muda wa wiki mbili sasa yanakabiliwa na ukosefu wa maji, bila serikali, kupitia kwa waziri husika, kutoa maelezo yanayoeleweka juu ya kadhia hiyo.

Maelezo yanayotolewa na serikali yanaonekana kujaa siasa zaidi kuliko uhalisia. Hivi nini kinashindikana kuwa na vyanzo vya uhakika wakati vipo na kwamba vinahitaji utashi tu na ukosefu wa maji katika maeneo mengi ya Tanzania itakuwa historia!

Inavyoonekana viongozi wengi, hasa wasaidizi wa Rais Samia (kama ilivyokuwa kwa marais wengi waliotangulia) hawana uchungu na madhila mengi yanayowakabili wananchi. Wao wakiteuliwa na kuapishwa, basi kazi kwao imeisha, na wananchi “watajiju.”

Ufike wakati sasa mawaziri na wasaidizi wengine wa rais wawekewe namna nzuri na yenye uwazi, kupima utendaji wa majukumu yao na wakishindwa waondolewe haraka.

MAMA NA BINTIYE...



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Jisca Magufuli, binti wa mtangulizi wake, John Magufuli mara baada ya kuhutubia wafuasi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakati wa shamrashamra za kuelekea kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wawili hawa walikutana Januari 10, mwaka huu katika Viwanja vya Maisara, Zanzibar. (Picha na Ikulu)

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.



*Kuna furaha ya wakati; ya muda mfupi, lakini pia ipo ya muda mrefu. Wale wa muda mrefu hujenga mazingira ambayo kwamba muda mwingi wanashughulika na mambo endelevu, yenye kuwapa matokeo wanayotarajia, yenye maana na yanayoongeza thamani katika maisha yao
- Balozi Khamis Suedi Kagasheki.*

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagua, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukaza Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamewekwa wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukituma mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandaa: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchagua, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscana

Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI

Logos: M-Pesa, Tigo, Airtel, Safaricom, etc.

Iweje CCM wajitwike mzigo wa ubaya?

Na Plato Hekimachus

VYOYOTE inavyoonekana, Chama Cha Mapinduzi (CCM), kinakabiliwa na changamoto nyingi ndani na nje.

Lakini, ninayoiona kubwa ni pale chama hicho tawala, kinapojitwika mizigo ambayo siyo yake, au ni yake, lakini chama chenye kinaamua kutoa ushahidi kuthibitisha kuwa mizigo hiyo mibaya ni yake.

Katika taifa hili, mtu akisimama hadharani akakemea wizi wa kura, CCM na makada wake wanakuja juu na kutukana, kutisha na hata kutumia vyombo vya dola kupambana na aliyekemea wizi wa kura.

Ni lini CCM itaacha kuonekana ni mwizi wa kura? Ni lini hata CCM itasimama hadharani na kukemea wizi wa kura na kutetea utawala bora wa sheria na haki?

Katika taifa letu, mtu akisimama akakemea vitendo vya upotoshaji wa haki na kutetea wanyonge wanaoonekana na mamlaka fulani, CCM ina tabia ya 'kuja juu' na kumpa mtu huyo majina mabaya.

Siyo mara nyingi kuona CCM ikimtetee mtu aliyeonekana na mamlaka. Ukiona CCM inatetee mtu ama ni mwana CCM au inatafuta kumfanya kuwa mwana CCM.

Mzigo huu siyo wa lazima kubebwa na CCM, lakini inaubeba kwa gharama ya kuonekana ni chama cha dhuluma, uonevu na ufsadi.

Ninaamini kwa dhati CCM inaweza kupata wanachama kwa kutetea haki na ukweli katika jamii.

Mtu akisimama hadharani katika taifa hili, akajenga hoja juu ya haja ya kuwa na katiba mpya inayojumuisha na kuunda miundombinu na taasisi huru za kidemokrasia, mtu huyo atapingwa kwa nguvu zote na CCM.

Kwa hiyo machoni pa wengi, CCM haitaki katiba mpya, haitaki demokrasia



Katibu Mkuu CCM - Dk. Emmanuel Nchimbi

ya kuendesha uchaguzi huru na wa haki.

Haitaki tume huru ya uchaguzi, haitaki msajiri huru wa vyama vya siasa, inatamani wagombea wasimamie uchaguzi na kujihesabia kura, kisha wajitangaze!?

Akitokea mtu akalalamika hadharani kuwa gharama za maisha zimepanda sana na watu wanashindwa kumudu mahitaji, tena mtu akaonyesha mpaka takwimu; CCM itampinga mtu huyo na kumtisha.

CCM itamwagiza rais wetu ambaye ni mwenyekiti wake, aruhusu polisi na jeshi kumsaka mtu huyo na kumtia adabu.

Hayo yanafanyika wakati gharama za maisha zilizopanda zinawatesa wana CCM na wasio wana CCM. Hivi chama kama taasisi, kwa nini kinafurahia mateso ya watu?

Akitokea mtu hadharani akatoa tuhuma za jumla au hata zenye ushahidi kuhusu rushwa na wizi wa mali ya umma, CCM humuita mtu huyo kumtisha au kumhoji kwa tishio la 'kumshughulikia.' Ingetegemewa kuwa mtu huyo angeungwa mkono au kupewa nishani ya ushujaa kwa kifichua hujuma kwa nchi.

Kwa nini CCM inakubali kirahisi kuonekana inawachukia wasema kweli na kuuchukia ukweli?

Akitokea kiongozi wa CCM anayatafuta kutenda kazi kwa haki, atavurugwa na chama na kutishiwa kuondolewa jina lake endapo atagombea nafasi yoyote.

Kwa nini inapotokea CCM kulemewa

Habari

Nani hasa anapanga kumuua Kigwangalla?

Na Peter ANDREA

MAISHA ya Mbunge wa Nzega, Dkt. Hamisi Kigwangalla, sasa yapo hatarini baada ya kuanza kufuatiliwa na watu “wasiojulikana.”

Wanaomfuatilia, inadaiwa kuwa wanataka “kumtoa roho” kwa kuwa amegusa maslahi yao, Pambazuko linaweza kueleza bila shaka.

Dkt. Kigwangalla ambaye amewahi kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, inadaiwa hivi sasa amekuwa akiishi kwa kujificha-ficha ili kuepusha watu hao kumdhuru.

Pambazuko limefuatilia tuhuma hizi ambazo zilifikishwa ofisini kwake na ndugu wa karibu wa daktari huyo wa tiba kwa binadamu, wakiomba dunia ijue ili kunusuru maisha ya daktari huyo, yanayoeleza kuwa “hatarini.”

Gazeti hili lilimtafuta Dkt. Kingwangalla ili kufahamu yeye anafahamu nini kuhusu kadhia hiyo ya “kuwindwa” na je, kuna sababu zozote anazohisi zimesababisha kusakwa ili “apotezwe.”

Dkt. Kigwangalla alisema hana uhakika nini hasa kinafanya afuatilwe na hata kuwepo kwa tishio la kumdhuru ama “kumpoteza kabisa.”

Mbuge huyo alisema pamoja na kushindwa kupata sababu hasa, lakini anahisi kuwepo kwa baadhi ya wale aliowaita “wakubwa” kukasirishwa na kauli yake kwamba – wapo baadhi ya viongozi wa serikali wenye utajiri wa kutisha, wakati ujira wao halali ni “kiduchu.”

Kigwangalla hata hivyo, amesema hajajua kina nani hasa wanamfuatikia, lakini amekuwa akichukua tahadhari na kujipanga kukabili kila anayemsogelea kwa nia ovyu.

Hivi karibuni, Dkt. Kigwangalla alionekana na kusikika akieleza kwamba wapo baadhi ya viongozi wa serikali wenye



Dk. Hamad Masauni, Waziri wa mambo ya ndani

ukwasi wa kutosha, ingawa mapato yao halali hayafikii utajiri mkubwa walionao.

Kigwangalla akisema; “wapo viongozi wa serikali, na wanasiasa, wameweza kununua majumba maeneo mahsusi, Dar es Salaam na hata nje ya nchi, lakini mishahara yao na maruurupu yao yote, hayafikii uwezo mkubwa wa kifedha na mali walizonazo.”

“Kuna kiongozi mmoja amenunua nyumba Masaki (Dar es Salaam) yenye thamani ya dola milioni sita, sasa unashangaa amepata wapi fedha hizi na amefanya kazi gani,” alihoji Kigwangalla.

Pamoja na kutotaja majina ya viongozi hao wa siasa na serikali, pia Kigwangalla alishangaa kuwepo kwa kiongozi mkubwa akiwa na nyumba maeneo mahsusi huko Dubai na mwingine katika moja ya majiji maarufu ya Marekani.

Mbali na kuwataja viongozi hao wa kisiasa hivi karibuni, Kigwangalla amekuwa katika mvutano na baaadhi ya wafanyabiashara wakubwa akiwatuhumu kuwa ni wanyonyaji na wakwepa kodi.

Kufuatilia tuhuma hizo, Kigwangalla pia ametumia kurada zake za mitandao ya kijamii, hasa X akieleza kadhia hii, huku akieleza kwamba “haogopi kitu, na hata kifo.”

Katika mtandao wake wa X juzi,
Inaendelea Uk. 10



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mezani kwa Chahali

Nchimbi atapikika vyema na Makonda?

HATIMAYE Dkt. Emmanuel Nchimbi ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM). Kwamba angeweza kuteuliwa kushika wadhifa huo siyo jambo la kushangaza kwani jina lake lilikuwa likitajwa mara kwa mara.

Tathmini hii ya kiintelijensia inaangalia, pamoja na mambo mengine, swali ambalo huenda watu wengi wanajuiliza - je “atapikika chungu kimoja” na Paul Makonda, Katibu wa Halmashauri Kuu (Itikadi, Uenezi na Mafunzo)?

Dkt. Nchimbi ni kada wa muda mrefu ndani ya CCM na yayumkinika kutanabaisha kuwa ni mtu sahihi kushika wadhifa huo.

Fursa nyingine kwa Dkt. Nchimbi ni ukweli kwamba yeye na makamu wa taifa wa chama hicho, Abdulrahman Kinana ni watu ambao “wametoka mbali pamoja kisiasa.” Kwa hiyo, suala la “teamwork” kwa wawili hao litakuwa siyo tatizo.

Kama ilivyo kwa Kinana, Dkt. Nchimbi amefanya kazi na makada mbalimbali wa muda mrefu wa chama hicho, na hao watamsaidia kwa kiasi kikubwa.

Lakini, pengine fursa kubwa zaidi kwake ni imani aliyonayo mwenyekiti wa taifa wa chama hicho, Rais Samia Suluhu Hassan, kwa katibu mkuu huyo mpya.

Hilo siyo gumu kubaini kwani inafahamika kuwa Rais Samia alikuwa anasaka katibu mkuu ambaye ni “mtu wake.”

Kwa upande mwingine, Dkt. Nchimbi anaingia madarakani huku CCM ikiwa haikabiliwi na “upinzani wa maana,” kwa sababu kimsingi, Chadema na ACT-Wazalendo hawajafanikiwa kutoa ushindani wa kutosha dhidi ya chama hicho tawala.

Na kwa kuwatendea haki, vyama hivyo viwili vimekuwa vikifanya kazi



Dkt. Emmanuel Nchimbi

katika mazingira yasiyo rafiki huku taasisi mbalimbali za umma zikifanya kazi kama vitengo vya CCM na kutotoa ushirikiano kwa wapinzani.

Na katika hilo la mazingira ya upinzani dhaifu, CCM ingeweza kabisa kufanya kazi bila hata kuhitaji katibu mkuu kwa sababu pamoja na ukweli kuwa mazingira hayajawahi kuwa rafiki kwa vyama vya upinzani, yayumkinika kuhisi kuwa vyama hivyo navyo ni kama vimekubali kuwa yanayowasibu ni stahili yao.

Sambamba na CCM kukabiliwa na upinzani dhaifu, Dkt. Nchimbi anaingia madarakani huku idadi kubwa ya Watanzania wakionesha kuwa “hawawezi kuishi bila CCM.”

Siyo kwamba Watanzania wengi wanaipenda CCM, bali wengi wao wana vipaumbele vingine – vingi vya hovyo - fursa ambayo CCM wanavitumia vizuri huku wapinzani wakihangaika kuhamasishana wao kwa wao.

Changamoto kubwa kwa Dkt. Nchimbi ni mwenezi wake, Makonda. Kama kuna mtu ambaye hana amani baada ya kusikia Dkt. Nchimbi ameteuliwa kushika wadhifa huo ni yeye, kwa sababu anafahamu fika kuwa katibu huyo mkuu mpya siyo kama mtangulizi wake, Daniel Chongolo ambaye Makonda hakuwahi kuficha dharau kwa boshi wake huyo.

Habari

Dakika 28, Tanesco yakata umeme mara 81

Na Mwandishi WETU

SHIRIKA la Ugavi wa Umeme Tanzania (Tanesco) jana lilizidisha mateso kwa wateja wake, hasa wa maeneo ya Bunju A, Dar es Salaam kwa kukata umeme mara 81, ndani ya dakika 28.

Umeme huo ulikatika kati ya saa 11:43 jioni hadi saa 12:11 jioni.

Gazeti la Pambazuko lililokuwa likifanya shughuli zake maeneo hayo, Barabara ya Mbweni, jirani na Shule ya Awali na Msingi ya Moga, lilikumbwa na adha hiyo, na baadaye, wakati hali hiyo ikiendelea, liliamua kukatiza kazi zake na kuondoka.

Wakati kadhia hiyo ikiendelea, Pambazuko lilipiga namba ya watoa huduma wa Tanesco, na simu iliita kwa muda wa dakika 4 bila majibu.

Katika muda huo simu hiyo ikiita, kulikuwa na muziki unaosifia shirika hilo la ugavi wa nishati hiyo muhimu ambayo sasa “inaonekana kuwa anasa nchini Tanzania.”

Wimbo huo ulisikika ukisifu kwamba – “Tanesco sasa linaangaza taifa - mijini hadi vijijini,” wakati ikifahamika kwa Watanzania wote, hata wasiopata huduma hiyo, kwamba “kuna mkwamo mkubwa” wa kupatikana kwa nishati hiyo muhimu.

Baada ya kusubiri kwa nne, simu ilipokelewa upande wa pili na mtu mmoja, mwenye sauti iliyosikika kuwa ya kiume iliitika na kujitambulisha kuwa mhusika anaitwa Adam Matata na kwamba anatoka makao makuu ya Tanesco.

Baadaye Adam aliomba kujua tatizo nini ili aweze kumhudumia mteja wake, hapo alipokea kilichokuwa kikitokea eneo hilo la Bunju A na kuahidi kutoa taarifa mahali panapohusika kwa ajili ya hatua.

Adam alisema; “ndugu mteja, pole sana kwa changamoto hiyo, naomba



Boss Tanesco - Boniface Gissima Nyamo-Hanga

kutoa taarifa mwa mafundi wetu na muda siyo mrefu watafika kwa ajili ya kutatua.”

Hata hivyo, hadi Pambazuko linaondoka eneo hilo, ili kwenda kubahatisha eneo jingine jirani lenye umeme, hali ilikuwa bado ikiendelea ya “zima –washa,” hatua ambayo ni hatari zaidi kwa usalama wa watumiaji wa nishati hiyo.

Hakuna taarifa ambayo Tanesco ilitoa kabla kwa wateja wao kwamba kutakuwepo katikakatika ya umeme, ili wajiandale na hata kuchukua hadhari kwa vifaa vyao vinavyotumia umeme.

Mmoja wa watu waliokuwa wakifanya kazi na Pambazuko, alisema kwa maneno machache kuhusu kadhia hiyo; “hawa Tanesco wameshindwa kazi.”

Hivi sasa, mara nyingi, Tanesco wamekuwa wakikata umeme bila kutoa taarifa na kwamba hatua hiyo imeleta madhara makubwa kwa wananchi kwa kuunguliwa vifaa vinavyotumia nishati hiyo ikiwamo majikofu, taa, televisheni, redio na vingine.

Hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, aliwaahidi Watanzania kwamba kadhia ya kukatika umeme mara kwa mara itapungua kuanzia February, mwaka huu baada ya kuanza uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Msilazimishe Samia kuonesha ‘rangi yake’

Na Rashid MTAGALUKA

ZIMBAKI siku chache Samia Suluhu Hassan atimize miaka mitatu tangu alipoapishwa kuwa Rais wa Tanzania - Machi 19, 2021, kufuatia kifo cha mtangulizi wake, Dkt. John Magufuli.

Mara tu baada ya kuapishwa, Rais Samia alifanya mabadiliko madogo ya uongozi kuanzia baraza lake la mawaziri na viongozi wengine wengi.

Tangu kuapishwa wasaidizi wake kwa mara ya kwanza, Rais Samia amekuwa akiteua na kutengua viongozi katika idara na wizara mbalimbali kila mara.

Rais Samia anachukua uamuzi huo, siyo kwa kujifurahisha tu, hapana! Bila shaka, ana lengo la kupata timu nzuri itakayomsaidia kutimiza jukumu kubwa la kuwatumikia Watanania kwa mujibu wa kiapo chake.

Katika hotuba zake mbalimbali, Rais Samia amejipambanua kwa kusema wazi kuwa yeye siyo msemaji sana kwa upande wa kwanza, na wala siyo kiongozi wa kutumia ‘maguvu’ kwa upande mwingine, ingawa anakiri kwamba, kwenye suala la uchapakazi hatofautiani na mtangulizi wake, ndiyo maana anasema “kazi indelee.”

Hata hivyo, inaonesha watendaji wengi wa serikali anayoiongoza, bado hawajamuelewa au wanamwelewa, isipokuwa wanatumia vibaya haiba ya upole wake na kujibaraguzwa kwa kutowajibika ipasavyo.

Maana kama siyo hivyo, wale viongozi wa Lindi walipata wapi ujasiri wa kuacha magari yalinyonunuliwa na serikali - yenye mitambo ya kuchimbia visima vya kuwasaidia wananchi kwenye matumizi ya nyumbani pamoja na kilimo cha umwagiliaji, yamejaa kutu bila kutumika?

Pia pikipiki zilizopelekwa Lindi na serikali tangu Juni, 2021, ili zikasaidie kutatua changamoto, lakini hazijagawiwa



Rais Samia akiapa

kwa wahusika, na hadi Januari, 2024 zilikuwa zimefungiwa chumbani zinapigwa vumbi tu!

Kutopewa wahusika ili wazifanye kazi wakati zinahitajika na kuziacha ‘zikioza’ ghalani, ni kielezo cha viongozi wabovu.

Kwamba, mkuu wa wilaya, katibu tawala wa wilaya, mkuu wa mkoa, katibu tawala mkoa, kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoa, pamoja na viongozi wengine mkoani Lindi, ni kweli hawakuwahi kuona tatizo hilo mpaka wamesubiri aende Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kuwaonesha?

Au tusema Lindi hakuna utamaduni wa kuwa na vikao vya chama ambavyo viongozi wa serikali husimama na kusoma utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ili kuonesha tija ya vitu vilivyoletwa na serikali kuu?

Kama vikao hivyo vipo, na viongozi husomeana utekelezaji wa ilani, kwanini viongozi wa CCM Lindi hawakubaini upesi kuwepo kwa uzembe wa viongozi?

Chonde viongozi wetu, kumbukeni nafasi mlizopewa kuwatumikia wananchi ni dhamana, siyo sadaka, rais ana imani kubwa na ninyi, msimlamizimhe kuona rangi zake halisi.

•**Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari anapatikana kwa simu namba 0784 438546 na barua-pepe:mtagaluka@gmail.com**

Habari

Iweje CCM wajitwike mzigo wa ubaya?

Inatoka Uk. 5

hoja na watu wanaoikosoa, huwa inakimbilia kutamba kwamba yenyewe ni chama cha 'mapinduzi,' na kwa hiyo haiwezi kuachia madaraka hivihivi kwa kutumia boksi la kura.

Na kwa nini CCM inapenda kujiweka nafasi ya Mungu kwa kudai ni ya milele? Waasisi wake wamekufa, uzalendo wake umekufa, miradi yake imekufa, lakini yenyewe inadai haiwezi kufa!?

Kwa nini CCM inachochea chuki katika nchi pale inapodhalilisha taaluma nyeti katika jamii? Mathalan, kutumia wanajeshi kuzoa taka, kutumia jeshi kununua na kusomba korosho, kutumia jeshi kusimamia uchaguzi na kuwahusisha katika wizi na hujuma za uchaguzi, kuteka badala ya kuokoa?

CCM inapofanya hayo ina uhakika gani

hao wanajeshi, wanafunzi na watumishi wa umma, hawawezi kuigeuka CCM na kuleta machafuko?

Kwa namna ya pekee na ya ajabu, watendaji wa CCM ndani ya chama na serikalini wanaojikuta wametenda makosa makubwa ya jinai kama mauaji, utekaji, utesaji, na hata uhalibifu wa mali za watu, hao hubebwa na chama kwa gharama zozote.

Chama huagiza watendaji wa serikali kuhakikisha wanasamehewa kwa sababu walitenda uhalifu wakikitetea chama.

Kama wahalifu hao wana kesi mahakama, basi waendesha mashtaka huenda wanaagizwa wahakikishe wanawaachia.

Baada ya kuachiwa, CCM huhakikisha wahalifu hao wanateuliwa tena ili kukitetea chama kwa njia za uhalifu uleule au mkubw zaidi.

Nani hasa anapanga kumuua Kigwangalla?

Inatoka Uk. 6

Kigwangalla ameandika kuwa amepata taarifa hizo za kutishiwa kuuawa na kuwa wapo watu wanamtafuta, ingawa hajawataja.

"Nimeambiwa kuwa nafuatiliwa, sijui kwa lengo gani, lakini naamini niko salama. Mnaoniuliza msiwe na shaka. Kama nikiitwa popote kwenye taasisi za seikali, ikiwamo Takukuru (taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa), tume ya maadili, Polisi, siyo mambo ya ajabu, huko ni mahala salama..."

... Nimekuwa nikishangaa na kushtuka, maana sina uadui na mtu, na sikutaja mtu. Kujaribu kuninyamazisha haitosaidia kitu, maana kama unahisi mimi najua kitu, ambacho sijakisema, jua na wengine wanajua...!

... Kama wewe ni kiongozi, jiulize tu

ukishaiba mali nyingi sana ya umma, unasikia raha gani? Utapeleka wapi? Utatumia zote hizo? Utazikwa nazo?

... Halafu jiulize, mwenye kosa ni anayetoboa mtumbwi ama anayepiga yowe na kumsonteshea mtoboaji ili wasafiri wote tushtuke? Tumdhibiti...?

... Kushtuka-shtuka namna hii inaonesha watu wanajishuku. Kunifuatilia na kutafuta kunitishatisha, mtanifanya nichambue hadharani taarifa za CAG (Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali; za Takukuru na michango ya wabunge bungeni, humo kuna viashiria vingi sana vya rushwa na ubadhirifu, je kama taifa mifumo yetu ya uwajibikaji imefanya kazi ipasavyo? Anahiji Kigwangalla.

Nilipozunguma juu ya uwepo wa haja ya kuimarisha mifumo ya uwajibikaji na usimamizi wa mali ya umma, sikuwa na nia ya kumtaja mtu yeyote...

Ukiwa Bukoba...

Furahia *Nowe* Freshi Juisi

Pata juisi (sharubati) ya matunda halisi iliyoandaliwa kwa usafi wa hali ya juu kwa kujali afya ya mteja.

Kunywa juisi ya:

Embe	Nanasi/pinacolada
Passion	Tende
Parachichi	Tikiti
Karoti	

Pia tunandaa juisi mchanganyiko maalum wa matunda ili kuondoa uchovu na magonjwa nyemelezi (detox) na pia smoothie.

Wasiliana nasi kwa namba hii:

0753949488



Habari

Makonda: Othman hataki kusikia ukweli

Na Tryruckia MFINANGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema kuwa Makamu wa Kwanza Rais wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar (SUK), Othman Masoud Othman, hataki kusema ukweli.

Msimamo huo umetolewa na Paul Makonda, Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM (Itikadi, Uenezi na Mafunzo), akijibu kauli ya Othman kwamba chama hicho tawala, hakijawahi kushinda “uchaguzi wowote Zanzibar.”

Othman ambaye ni makamu mwenyekiti wa chama cha ACT - Wazalendo (Zanzibar) alisema mara zote kinachofanwa na CCM, tangu uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi vya siasa mwaka 1995 ni unyang’anyi, hadaa na ubabe.

Akizungumza na Pambazuko, Makonda alisema Othman ameng’ang’ana na kile alichoeleza kuwa ni uongo wa chama chake na vingine vya upinzani, kulaumu matokeo badala ya kulaumu wapiga kura wao.

“Zamani tulikuwa tunasema sisi, lakini sasa hivi mmekwishawasikia viongozi wenyewe wa Chama Cha Mapinduzi, wanasema CCM haijawahi kushinda Zanzibar, kinachotumika ni nguvu, ghaliba na hadaa katika uchaguzi” alisema Othman

“Leo tupo ndani ya serikali si kwa bahati mbaya, tuko ndani ya serikali kwa sababu wenzetu walifika mahala wakakubali ukweli, kwamba angalau tuweze kuwa nao pamoja tuwazoe kabla hatujawapa serikali, “ aliongeza kiongozi huyu.

Othman alitumia fursa hiyo akizungumza na wanachama wa chama chake huko Mkoa wa Ruvuma kuwaeleza kuwa uchaguzi ujao, chama chao kitashinda Zanzibar.

Makonda alisema vyama vya upinzani vimeshatambulika kwa wananchi, kwamba vinazungumza bila kuwa na ushahidi, hivyo wananchi wanawakataa



Paul Makonda

kwa kupitia sanduku la kura.

“CCM inaheshimika, inaaaminika na zaidi kabisa, inatambua wananchi wanataka nini, ndiyo maana wanaichagua kila kunapofanyika uchaguzi,” akaongeza Makonda.

Othman, mara kadhaa amekuwa akiwahakikishia Watanzania kwamba yupo katika nafasi hiyo kisheria na siyo kwamba anafurahia mambo yanayofanywa na serikali ya sasa, inayoongozwa na Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

“Msije mkadhani niko hapa kwa kuvutiwa na umakamu wa rais, hapana, mimi nilikuwa nafanyakazi serikalini, nikiwa mwanasheria wa kawaida, mwanasheria mkuu na Katibu Mkuu wa Wizara ya Sheria kwa miaka tisa, nikawa mkurugenzi wa mashtaka, mwanasheria mkuu kwa miaka minne na mimi ndiye nilianzisha chombo cha kukusanya mapato Zanzibar kwa sasa Mamlaka ya mapato Zanzibar.

“Sikuvutiwa na maslahi ya mwanasheria mkuu, niliwaambia mimi siyo mwanasheria mkuu wa CCM, si mwanasheria mkuu wa aliyeniteua, bali mimi ni mwanasheria mkuu wa Wazanzibari ili kulinda nafasi na maslahi yao na kama naona maslahi yao hayatimizwi huu uanasheria mkuu hautimii, nikakubali nikatoka.” alisema Othman.

Othman amerithi nafasi hiyo baada ya kufariki dunia kwa Maalim Seif Shariff Hamad Machi 2021.

Ndoto ikitimia, Mwinyi ataacha alama

NA Jabir IDRISSA

UTIAJI saini mkataba wa ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri, kilomita tano kutoka Bandari Kuu ya Malindi, unaashiria kupatikana ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la muda mrefu la msongamano kwenye bandari ambayo ni mhimili mkuu wa uchumi

Bandari ya Malindi yenye historia ya zaidi ya miaka 200, imekuwa na ufinyu wa nafasi ya kukaa abiria wanaosubiri kusafiri kwenda Dar es Salaam na Pemba ambako hufikia Bandari ya Mkoani Kusini Pemba na bandari ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Upande wa kusafiri abiria mara nyingi utakuta msongamano mkubwa hasa pale boti za kampuni mbili tofauti zinapokutana kwa ajili ya kupakia au kushusha abiria.

Kwenye eneo hili la meli za abiria za aina ya pantoni na zile boti za mwendokasi, ikitokea boti mbili kuegesha, moja kila upande wa lilipo gati maalum la kupandia na kushukia, hakuna tena nafasi ya meli/boti nyingine kuegesha.

Ukigeukia Bandari Kuu ya Malindi inayotumika zaidi kwa ajili ya meli kubwa za mizigo kutoka ughaibuni, nafasi yake haitoshelezi mahitaji halisi wakati huu nchi ikiwa inapokea shehena kubwa zaidi.

Hili ni tatizo linalochofisha ukuaji wa sekta ya usafiri na usfirishaji mizigo na hivyo kuinyima serikali mapato inoyahitaji sana kukuza uchumi wake.

Tatizo linalozaa matatizo ni donda ndugu ambalo serikali hajafanikiwa kuliiondoa licha ya ahadi na mipango mingi. Ndio eneo ambalo tangu Novemba mwaka jana, hatimaye serikali iliingiza mwekezaji wa kigeni kampuni ya Kifaransa ya African Global Logistics (AGL), inayohudumia sehemu ya meli za mizigo mikubwa.



Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi

Ufinyu wa nafasi kwenye eneo hilo pia umekuwa ukiumiza akili za viongozi wa viongozi wa serikali na alipoingia Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi amekiri ukubwa wa tatizo.

Akizindua boti mpya ya Kilimanjaro VIII ya kampuni ya Azam Marine Fast Ferries, Aprili mwaka jana, Rais Mwinyi alisema mipango ipo mbioni kupata ufumbuzi, ahadi iliyopata kutolewa na watangulizi wake.

Hatimaye muarubaini umepatikana. Angalau serikali anayoongoza imefanikiwa kupata fedha za kujengea Bandari ya Mpiga Duri ambayo imekuwa ikitajwatajwa, lakini ahadi za kujengwa zikibakia ndoto.

Kwa mujibu wa maelezo ya Dkt. Mwinyi, ujenzi wa bandari hiyo utakaochukua miezi 36 (miaka mitatu) chini ya ukandarasi wa kampuni ya ZF Devco ya Uholanzi utakuwa ukombozi kwelikweli.

Mkataba huo utahusisha ujenzi wa eneo la boti za abiria, meli ndogo za mizigo, taksi za baharini, maduka ya kisasa, ndege za baharini, kituo cha umma cha usafiri wa mabasi, hoteli ya nyota tano, ukumbi wa kimataifa wa mikutano na eneo la maegesho ya boti.

Habari katika picha



Rais Samia Suluhu Hassan akimpongeza Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kiluthero Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa baada ya kuingizwa kazini wakati wa Ibada Maalum iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Azania Front, jijini Dar es Salaam jana. (Picha zote na Ikulu).



Baadhi ya wachungaji wakiwa kwenye Ibada Maalum ya kumingiza kasini, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kiluthero Tanzania (KKKT) Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa inayofanyika kanisani hapo jijini Dar es Salaam jana.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza jambo na watoto waliohudhuria Ibada Maalum ya Kumingiza kasini Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kiluthero Tanzania (KKKT) Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa iliyofanyika jana.



Viongozi mbalimbali wakiwa kwenye Ibada Maalum ya kumingiza kasini, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kiluthero Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa inayofanyika jana.



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Kenya

Kenya yasema haina vita na majirani

Na Mwandishi WETU

WAZIRI Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Kenya, Musalia Mudavadi ametupilia mbali uvumi kwamba nchi yake iko katika mzozo na majirani zake.

Mudavadi ameviomba vyombo vya habari kuacha kupaisha habari hizo kwa kuwa hazina ukweli wowote, isipokuwa zinaonekana kubeba nia ovu dhidi ya nchi hiyo ya Afrika Mashariki.

Akizungumza jana mjini Busia, kwenye hafla iliyohudhuriwa na Rais William Ruto, Mudavadi alisema Kenya badala yake imekuwa mstari wa mbele kutetea amani katika eneo la Afrika Mashariki.

“Kenya haina vita na majirani zake. Kwa hakika Rais Ruto yuko mstari wa mbele kuleta amani katika eneo hili. Kuna nchi zinazozana na rais wetu amedhamiria kuona amani inatawala katika nchi hizi, kwa sababu wakipigana, basi vita vitatufikia sisi pia,” aliongeza Mudavadi.

Maoni yake yanakuja huku kukiwa na madai ya mvutano kati ya Kenya na baadhi ya majirani zake, hasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Wiki iliyopita, Tanzania ilisitisha safari za shirika la ndege la Kenya, Kenya Airways (KQ), kuingia anga la Tanzania kwa kile kilichodai kuwa ni kulipiza kisasi kwa Kenya kukataa ndege zake za mizigo kufanya kazi kutoka Nairobi.

Mgogoro huo ulitatuliwa haraka wakati Kenya ilipokubali kuruhusu ndege za mizigo za Tanzania kufanya kazi kutoka Nairobi.

Katika tukio jingine, Uganda iliishtaki Kenya katika Mahakama ya Afrika Mashariki baada ya nchi hiyo kuinyima leseni Shirika la Mafuta la Uganda ya kufanya kazi nchini humo.

Aidha, katika tukio jingine - mwezi



Musalia Mudavadi

mmoja uliopita, DCR ilimrejesha balozi wake DRC nchini Kenya baada ya muungano mpya wa waasi wa Congo kusemekana umeundwa mjini Nairobi.

Muungano mpya wa rais wa zamani wa Tume Huru ya Kitaifa ya Uchaguzi (Ceni), Corneille Nangaa, unaonekana kuwa tatizo kuu dhidi ya usalama wa taifa huko DRC.

Kenya ni mwanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC), ikiwa ni moja ya nchi saba zinazounda kundi hilo, nchi nyingine ni Jamhuri ya Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Jamhuri ya Kenya, Jamhuri ya Rwanda, Jamhuri ya Sudan Kusini, Jamhuri ya Uganda, na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Makao ya Jumuia hiyo yako Arusha, Tanzania.

Mkutano wa EAC uliikubali Jamhuri ya Shirikisho ya Somalia katika Jumuia ya Afrika Mashariki Novemba 24, 2023.

Jamhuri ya Shirikisho ya Somalia itakuwa mwanachama kamili pindi hati za kuridhia Mkataba wa EAC zitakapopokelewa na katibu mkuu wa umoja huo.

Museveni mwenyekiti mpya wa G77

Na Mwandishi WETU

RAIS Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda, amepokea kijiti cha uongozi wa Jumuia ya Matifa Machanga 77 yaliyoko Kusini mwa Ikweta, akianza kwa kuongoza mkutano wa wakuu wa nchi hizo unaoendelea mjini Kampala, tangu tarehe 21 Januari mwaka huu.

Akiongea katika mkutano huo, Rais Museveni alihimiza mageuzi katika mifumo ya taasisi za fedha za kimataifa, ili ziweze kuzinufaisha nchi zilizo Kusini mwa Ikweta.

“Kwa maoni yetu, taasisi za fedha za kimataifa na benki za maendeleo za kimataifa zinawajibika kufanya mageuzi yatakayoziwezesha kuunga mkono vipaumbele vya kitaifa vya nchi zinazoendelea, bila kuweka masharti yoyote ambayo yanakiuka uhuru wao,” amesisitiza Museveni.

Kiongozi huyo wa Uganda alisisitiza umuhimu wa kuhakikisha kuwa hakuna nchi inayoachwa nyuma na akahimiza kukabiliana na changamoto zinazokabili nchi zilizo katika mazingira magumu.

Rais Museveni aliitaja Afrika, kuwa na nchi nyingi zenye mazingira magumu na zilizo nyuma kimadalea (LDCs), nchi zinazoendelea na ambazo hazipakani na bahari (LLDCs), nchi zinazoendelea na ambazo ni visiwa (SIDS), nchi za kipato cha kati, nchi zenye migogoro na zilizoondokana na migogoro hivi karibuni, na nchi zilizo chini ya utawala wa kigeni.

Museveni alisisitiza umuhimu wa umoja ndani ya Kundi la Mataifa 77 (G77) katika kutafuta maslahi ya pamoja katika Umoja wa Mataifa na kuwataka wanachama kuendelea na kutetea vipaumbele vya kundi hilo katika michakato ya kiserikali.

Kundi la G77 lilianzishwa mwaka 1964 katika kikao cha kwanza cha



Rais Yoweri Museveni

Kongamano la Biashara na Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNCTAD). Lengo lake ni kushughulikia changamoto za maendeleo ya kimsingi zinazozikabili nchi hizi katika mfumo usio wa haki wa kiuchumi duniani.

Hivi sasa, mataifa 77 pamoja na China zinawakilisha asilimia 80 ya idadi ya watu ulimwenguni, na pato la taifa la kila nchi likielezwa kuwa ni zaidi ya asilimia 40.

Kupitia hotuba yake kwenye mkutano wa tatu wa wakuu wa nchi za hizo 77, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres alishukuru Serikali ya Uganda kwa ukarimu wake, na kuipongeza kwa kushika kijiti cha uongozi wa mataifa hayo.

Katibu huyo mkuu aliwakumbusha wanachama wa Mataifa 77 kuwa, wakati dunia ikiwa katika nusu ya tarehe ya mwisho ya 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu, ambayo kauli mbiu yake ni “kutomwacha mtu yeyote nyuma,” ukweli ni kwamba, badala ya kutomwacha mtu yeyote nyuma, leo tumeiacha nyuma nusu ya dunia.

“Ni lazima kuongeza kasi kuelekea shabaha za Malengo ya Maendeleo Endelevu,” alisisitiza Katibu wa Umoja wa Mataifa.

DR Congo

Walinzi UN waanza kuondoka DRC

Na Mwandishi WETU

BAADA ya miaka 25 ya kufanya kazi ya kulinda amani ndani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), sasa walinzi wa hao wa Umoja wa Mataifa (UN) wameanza kuondoka katika nchi hiyo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa DRC, Nje Christophe Lutundula, alitangaza Jumamosi iliyopita kwamba operesheni hiyo inastahili kukamilika mwishoni mwa mwaka huu.

Akizungumza pamoja na viongozi wa Kikosi cha Umoja wa Mataifa cha kulinda Amani (Monusco), waziri huyo aliuambia mkutano na waandishi wa habari kwamba watafanya kazi ya kujiondoa kwa kutumia mkakati wa kiufundio.

Monusco leo ina wanajeshi 13,500 na polisi-jeshi 2,000, wengi wao kutoka nchi za Asia na Afrika, katika majimbo matatu ya mashariki ya ya DRC ambayo ni Ituri, Kivu Kusini na Kivu Kaskazini.

Kuondoka kwa wanajeshi hao kunatarajiwa kufanyika katika awamu tatu, ambapo UN itahakikisha usalama wa uhakika wa wapiganaji hao. Kundi la kwanza litaanza kuondoka mwishoni mwa Aprili, mwaka huu.

Licha ya ghasia zinazoendelea mashariki mwa DRC, serikali ya nchi hiyo imekuwa ikitoa mwito kwa miezi kadhaa kuondoka kwa walinda amani hao, ambao walitumwa nchini humo kwa mara ya kwanza mwaka 1999.

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilipiga kura mwezi Desemba mwaka jana kutekeleza maombi ya DCR kutaka wanajeshi hao kuanza kuondoka.

DRC pia imekataa kurejesha wanajeshi wa Kikosi cha Kanda ya Afrika Mashariki, ambacho kilianza kuondoka Desemba 2023.



Katibu Mkuu UN- Antonio Guterres

Viongozi wa nchi ya DRC wanaona kuwa vikosi vya kimataifa havina ufanisi kuwalinda raia dhidi ya makundi yenye silaha na wanamgambo ambayo yamekuwa yakikabili mashariki mwa DRC kwa miongo mitatu sasa.

Katibu Mkuu wa Monusco, Bintou Keita, amesema baadhi ya kambi za jeshi hilo la UN huko Kivu Kusini, zinatarijiwa kuanza kufungwa ifikapo Februari 15 mwaka huu na kukabidhiwa kwa vikosi vya usalama vya DRC.

Aliahidi kwamba kituo cha kwanza kukabidhiwa kipo kwa mamlaka ya DRC kiko eneo la Kamanyola mpakani mwa nchi hiyo na Burundi.

Lutundula alisema anatarajia mchakato huo kukamilika ifikapo tarehe 31 Desemba mwaka huu. “Tunapigania kila kitu kifanyike mwishoni mwa mwaka huu,” alisema.

“Kuondoka huko hakumaanishi mwisho wa vita,” waziri wa mambo ya nje alisema na kuendelea kusesitiza kwamba amani kupatikana kutategemea zaidi kukomeshwa kwa “misaada kwa waasi” hasa kwa kundi la M23 kutoka baadhi ya nchi jirani.

Wakimbizi Rwanda marufuku Uingereza

Na Mwandishi WETU

BUNGE la Uingereza limeidhinisha muswada wa kuwanyima hifadhi wakimbizi wa kisiasa kutoka Rwanda, kwa sababu ya hoja kwamba sasa nchi hiyo ni salama.

Novemba mwaka jana - 2023, Mahakama Kuu ya Uingereza ilitupilia mbali muswada wa awali kuhusu wakimbizi kutoka Rwanda baada ya mahakama hiyo kuamua kuwa Rwanda haikuwa nchi salama kwa wanaotafuta hifadhi.

Uamuzi huo wa mahakama ulimfanya Waziri Mkuu wa Uingereza, Rishi Sunak, ambaye ni kiongozi wa chama cha kihakafidhina, kuwasilisha upya bungeni muswada wake.

Muswada huu mpya ulikusudiwa kuifanya iwe vigumu kwa mahakama kupinga sheria yake kwa kulitaka Bunge kutangaza kwa kura nyingi kwamba Rwanda ni nchi salama kwa wananchi wake wanaotafuta hifadhi ughaibuni.

Waziri Mkuu Sunak aliwasilisha muswada wake mpya bungeni Desemba mwaka jana, lakini ilibidi ashindane na wabunge wenye misimamo mikali ya mrenjo wa kulia kutoka chama chake ambao walidai kuwa muswada huo bado haukuwa na ushahidi wa kutosha.

Mwishowe, kiongozi huyo alipata kura nyingi za kuunga mkono muswada wake baada ya wapinzani wake, ambao wengi wao walikataa kuamua kuruhusu sheria hiyo kupita kwa matumaini.

Waziri Mkuu Sunak alifaulu kushinikiza muswada wake wa hifadhi na uhamiaji kupitia bunge baada ya 'uasi' uliotarajiwa wa wabunge wa chama cha Conservative kutokomea.

Baadhi ya wabunge kutoka chama cha Sunak wenyewe walitishia kupiga kura dhidi ya muswada wa "Usalama wa Rwanda" kwa misingi kwamba mipango



Rais wa Rwanda Paul Kagame

ya serikali ya kutuma baadhi ya waomba hifadhi nchini Rwanda haikuwa imara vya kutosha kustahimili changamoto za kisheria.

Lakini mwishowe, ni wabunge wahafidhina 11 pekee wenye msimamo mkali walioasi na sheria ikapitishwa kwa uwiano wa kura 276 dhidi ya 320.

Muswada huo sasa utahamishiwa kwenye Bunge la Juu la Uingereza, House of Lords, ambalo litajadili na kupiga kura juu ya sheria hiyo. Bado Bunge hili linaweza kuzuia au angalau kuchelewesha muswada huo.

Sheria ya kuwalinda wahamiaji kutoka Rwanda kwenda Uingereza ilitangazwa kwa mara ya kwanza na Waziri Mkuu wa zamani, Boris Johnson Aprili 2022.

Miezi miwili baadaye, Juni, 2022, safari ya kwanza ya ndege iliyokuwa ikielekea Rwanda kutoka Uingereza ilipaswa kuondoka na waomba hifadhi, Ilistishwa.

Safari hiyo ilizuiwa katika dakika za mwisho baada ya Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu (ECHR), ambayo iliamuru kwamba mmoja wa watu wanaotafuta hifadhi, alikuwa katika hatari halisi ya madhara yasiyoweza kurekebisha ikiwa angerejesha nchini Rwanda. ends

Zitto ni mkulima pia...



Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, juzi- Januari 20, alipita shambani kwake, Kijiji cha Matyazo, Kata ya Kalinzi, Kigoma Vijijini kwa lengo la kutazama ukuaji wa miche ya kfsasa ya kahawa. Pamoja na shughuli zangu za kisiasa, Zitto ni mkulima. (Picha kutoka mtandao wake wa X).

GAZETI hili lilianshwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaandeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

